



Bwana Kio anaishi  
kijijini kwetu. Ana paka  
anayeitwa Safi.



Bwana Kio anapoenda  
kazini, anauacha  
mlango wazi.




Safi anaketi mlangoni  
na kuilinda nyumba.



Mbwa wa jirani  
akiikaribia nyumba,  
Safi anamtisha.

Yuko tayari  
kumkwaruza kwa  
kucha zake.



Mbwa anatoroka na kurudi kwao.



Jirani akiugusa  
malango wa nyumba,  
Safi anamwona. Yuko  
tayari kumkwaruza.



Jirani anageuka haraka  
na kwenda zake.



Safi anapohisi njaa,  
anajua la kufanya.  
Anaufunga mlango,  
kisha anaenda kula.





Safi anakula kutoka  
bakuli lake la bluu.  
Anakipenda chakula  
chake sana.



Akimaliza, anaruka juu  
ya sofa na kulala.  
"Purr! Purr! Purr!"



Bwana Kio anarudi  
nyumbani jioni.  
Safi anajinyoosha kwa  
furaha na kumlaki.



Bwana Kio na Safi wanaketi sebuleni. Kila mmoja anasoma gazeti.